Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Kwanza - Tarehe 13 Aprili, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mkutano wa Kumi na Tano, Kikao cha Kwanza kinaanza.

Lakini kabla hatujaanza nitoe maelezo kuhusu ratiba ya leo kama inavyoonekana kwenye *Order Paper* ni kwamba kwa kuwa jana hatukuweza kufanya ule Mkutano wa Wabunge wote kama kawaida yetu kwa ajili ya kupata maelezo mbalimbali na kubadilishana mawazo, tumepanga kwamba huo Mkutano ambao tunauona ni muhimu ufanyike leo.

Kwa hiyo, ratiba itakuwa ni kwamba baada ya Maswali na Majibu, Bunge litaahirishwa mpaka saa 11.00 jioni ndipo tuanze shughuli za Miswada ya Sheria. Kikao kinaanza Katibu.

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):**

Nakala za Matoleo yote ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 1

**Mawaziri/Manaibu Kutouliza Masuala yao Bungeni**

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa kipindi kifupi nilichokuwa ndani ya Bunge nimejifunza mambo mengi na kati ya yale niliyojifunza ni lile la Mawaziri na Manaibu kutouliza masuala ya wananchi wanaowawakilisha Bungeni:-

(a) Je, ndio kusema kwamba huo ndio utaratibu waliowekewa?

(b) Je, wao huwa wanawakilisha vipi wapiga kura wao wakiwa kama Wabunge, kwa maana ya hoja na matatizo ya Majimboni mwao huwa yanatatuliwa vipi?

(c) Je, kwa njia hiyo watakuwa wanawatendea/tunawatendea haki kwa kiasi gani wananchi husika?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mbunge wa Matemwe, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mawaziri na Manaibu Waziri wana masharti yao ya kazi sambamba na yale ya Ubunge. Viongozi hawa ndiyo watekelezaji wakuu wa Sera na Ilani ya Chama Tawala (CCM). Aidha, hupokea kero na hoja za wananchi kupitia Waheshimiwa Wabunge na kuzijibu kwa makini kupitia majibu ya maswali hapa Bungeni, Hotuba za Bajeti, barua au kuwasiliana ana kwa ama na Waheshimiwa Wabunge na pia hutembelea Mikoa, Wilaya na maeneo husika ili kutatua na kukutana na wananchi moja kwa moja.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge, kuwa Mawaziri na Manaibu Waziri hutekeleza kazi za Serikali kama timu moja na Serikali kujiuliza maswali rasmi yenyewe haina mantiki. Wanachopaswa kufanya ni kutumia vikao maalum hususan kama vikao vya Baraza la Mawaziri ambapo maamuzi mengi muhimu hujadiliwa kuwasiliana kwa maandishi au ana kwa ana baina yao.

(c) Mheshimiwa Spika, Mawaziri na Manaibu Waziri hupata fursa ya kuzungumza na wananchi na kujibu maswali wakati wa vikao vya Chama na Serikali au Mikutano ya hadhara katika Jimbo lake la uchaguzi wakati wa ziara rasmi huko.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Mawaziri na Manaibu Waziri, ni watekelezaji wa maamuzi ya Serikali na ushauri na Manaibu Waziri ni watekelezaji wa maamuzi ya Serikali na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge kwa nchi nzima na siyo kwa Majimbo yao ya uchaguzi peke yao. Wanaweza kutoa ufafanuzi na ushauri mahali popote na kwa jambo lolote lenye manufaa kwa Taifa.

Na. 2

**Redio na Televisheni Binafsi Kurusha Matangazo Nchini Kote**

**MHE. BAKARI M. MBONDE** aliuliza:-

Kwa kuwa sasa Redio na Televisheni binafsi nchini zimeruhusiwa kurusha matangazo na kuonekana kote nchini.

Je, Serikali imejiandaa vipi ili Televisheni ya Taifa *(TVT)* iweze kushindana na Televisheni nyingine kwa ubora na aina ya vipindi vyake kwa lengo la kukidhi matarajio ya rika mbalimbali za watazamaji?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Mbonde, Mbunge wa Rufiji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sera na Utangazaji ya mwaka 2003 imetoa fursa kwa vyombo vyote vya habari vitakavyokuwa vimesajiliwa na kukubalika kwa mujibu wa sheria, kurusha na kuweza kufikisha matangazo nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko hayo yanalenga kutoa wigo mpana na pia kutoa ushindani sawa kwa vyombo vyote vya binafsi na Serikali katika kupata na kutoa habari. Ili kuhimili ushindani, Serikali imejitahidi kwa sasa kufanya yafuatayo, kwa Redio na Televisheni ya Taifa.

Kwanza, Serikali imeanzisha Taasisi ya Utangazaji Tanzania *(TUT)* ambayo ni muungano wa Redio na Televisheni na kusimamiwa na chombo kimoja. Lengo ni kuunganisha vyombo hivi ni kuviongezea uwezo wa kutumia raslimali na miundombinu iliyopo kwa ushirikiano mkubwa.

Pili, katika kuunganisha Redio na Televisheni pia wafanyakazi wa Redio hasa walioko Mikoani wataweza kutumiwa na Televisheni ya Taifa katika kukusanya na kusambaza habari kwa vyombo vyote viwili. Aidha, vipindi vingine vitaweza kutengenezwa kwa urahisi kwa kutumia wafanyakazi hao.

Tatu, kuanzia mwezi huu wa Aprili, 2004 Televisheni ya Taifa imeongeza muda wa matangazo yake kwa saa tatu na hivyo kutangaza kwa muda wa saa 12. Muda huu utaongezwa tena ifikapo tarehe 1 Julai, 2004 kwa kutangaza saa 18 yaani kuanzia saa 12 asubuhi hadi saa 6 usiku.

Mheshimiwa Spika, nne, pamoja na matarajio hayo, kupatikana na vipindi bora kunategemea pia uwezo wa Taasisi hiyo katika kupata vifaa na teknolojia ya kisasa ili

iweze kushindana na vyombo vingine. Jitihada zinafanywa kupata vifaa hivyo pamoja na mitambo ili waandaaji vipindi waweze kuwa na nyenzo bora za kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, tano, kadri ya hali ya fedha inapoimarika wafanyakazi wenye taaluma wataajiriwa ili kuandaa vipindi bora kwa Televisheni ya Taifa.

**MHE. BAKARI M. MBONDE:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba katika kipindi cha hivi karibuni *TVT* imeonyesha uhai na ubora mkubwa katika vipindi vyake. Lakini nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Je, isingekuwa vizuri kwa *TVT* sasa kusambaza dodoso kwa watazamaji wake ili waweze kushauri aina na muda wa vipindi ambavyo wanatazama hawa watazamaji? *(Makofi)*

(b) Je, isingekuwa vizuri kwa *TVT* kwa sababu kuna wapenda michezo wengi kwamba ingeanza kuonyesha michezo inayochezwa hapa ndani iwe ni Ligi Kuu ya hapa ndani au michezo ya Kimataifa kama vile *soccer* ili watazamaji wake waweze kuona moja kwa moja kama ambavyo zinavyofanya Televisheni za Taifa za nchi zingine? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Mbonde, Mbunge wa Rufiji, kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza ni la msingi anasema kwamba kuna uwezekano wa kupeleka dodoso kwa watazamaji, inaruhusiwa wananchi kutoa maoni yao ili kuimarisha vipindi vya Televisheni. Kwa hiyo, Mheshimiwa Bakari Mbonde na wengine wanaruhusiwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, la pili kuhusu kuonyesha mashindano ya mpira wa ndani inafanya hivyo *TVT,* imeonyesha mpira wa Simba na *Club* moja ya nje lakini hivi karibuni mnafahamu Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali imeruhusu *TVT* kuonyesha Kombe la Afrika na *Clab* Bingwa ya Afrika pia itaonyesha ambayo gharama zake ni kubwa kidogo zaidi ya shilingi milioni 69.

Kwa hiyo, ni gharama kubwa sana lakini hata hivyo Serikali itajitahidi *TVT* ionyeshe mashindano hayo ili wananchi wa Tanzania wafaidike na uhondo huu wa michezo. *(Makofi)*

Na. 3

**Barabara ya Kyabakari - *Ikoma Gate***

**MHE. TEMBE K. NYABURI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali katika kujibu swali Bungeni mwaka 2001/2002 na 2003/2004 swali Na. 276 la Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, ilisema kwamba ina nia ya kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Kyabakari - Butiama - Nyamuswa - *Ikoma Gate,* lakini majibu ya Serikali mara zote yamekuwa kwamba uwezo utakaporuhusu.

(a) Je, Serikali inafahamu kwamba kama barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami itafungua mlango wa Utalii katika Kanda ya Ziwa?

(b) Je, ni lini Serikali itaanza kutafuta na kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo badala ya kuendelea kuimba wimbo wa hadi hali itakaporuhusu ambao unawakatisha tamaa wananchi wa maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tembe Kerenge Nyaburi, Mbunge wa Bunda, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kurudia kusema kwamba Serikali bado ina msimamo ule ule wa kuijenga barabara yote ya kutoka Kyabakari - Butiama - Nyamuswa - *Ikoma Gate* kwa kiwango cha lami. Hii ni kwa kutambua umuhimu wa barabara hii kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi wa Mkoa wa Mara na Taifa hili kwa ujumla. Tatizo tulilo nalo ni ukosefu wa fedha za kutekeleza kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi hii ni kubwa sana na mtandao wa barabara zake ni mkubwa kiasi kwamba kulingana na uwezo wetu kiuchumi, kuzihudumia barabara zote kwa wakati mmoja ni vigumu. Hivyo utekelezaji wake umepangwa kufanyika kwa awamu kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza ya sehemu ya Kyabakari - Butiama ya kuweka makalvati pamoja na kunyanyua tuta sehemu yaliyojengwa makalvati kwa gharama ya shilingi 714,000,000/= imekamilika mwaka 2002. Mkataba wa awamu ya pili ya ujenzi wa tuta lote sehemu ya Kyabakari - Butiama na kuweka tabaka la lami wenye thamani ya shilingi bilioni 2.08 ulisainiwa tarehe 16 Januari, 2004 kati ya *TANROADS* na Mkandarasi *China Henan International Corporation Group Co. Ltd. (CHICO).* Kazi zimeanza mwezi Machi, 2004 na zinatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2005.

Aidha, sehemu kubwa ya barabara hii ya makutano - Butiama - Nyamuswa hadi *Ikoma Gate* kwa hivi sasa inaendelea kufanyiwa matengenezo kwa kiwango cha changarawe chini ya mradi wa *El-Nino Infrastructure Repairs* unaofadhiliwa kwa mkopo toka Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* na sehemu zingine zinafanyiwa matengenezo chini ya Meneja ya Mkoa *TANROADS* kwa fedha za *Road Fund.*

Tunaamini baada ya matengenezo hayo kukamilika barabara hii itakuwa inapitika kwa urahisi sana wakati juhudi za kutafuta wafadhili kwa ajili ya ujenzi kufikia kiwango cha lami kwa sehemu iliyobaki zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelekezo hayo naamini Mheshimiwa Tembe Nyaburi, Mbunge wa Bunda, ameona juhudi inayofanywa na Serikali katika kuondoa kero za wananchi kwa kujitahidi walau kwa uwezo mdogo uliopo kiuchumi kuziwezesha barabara zote muhimu kwa uchumi wa nchi hii kuwa katika hali ya kupitika.

**MHE. STANLEY H. KOLIMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Kamati ya Fedha na Uchumi ilipitia eneo la Butiama mwaka jana na kuona hali ilivyo ya barabara ile, je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza barabara kutoka Mbuga za Ngorongoro kupitia Kaburi la Mheshimiwa Baba wa Taifa, ili paweze kupitika kwa uhakika zaidi?

**SPIKA:** Hilo ni swali jipya lakini kama una majibu Naibu Waziri yatoe, huna basi tunaendelea, ni swali jipya liletwa kwa taratibu za kawaida. Swali linalofuata Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo.

Na. 4

**Fedha za Mfuko wa Barabara**

**MHE. DR. AARON D. CHIDUO** anauliza:-

Kwa kuwa Serikali imekuwa inapeleka fedha Mikoani kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara za Mikoani na Wilayani kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara.

(a) Je, Serikali imeweka utaratibu gani wa kuainisha barabara zinazostahili kupatiwa fedha kila mwaka?

(b) Je, Serikali inao utaratibu gani wa kujua kwamba fedha hizo zinakwenda kwenye maeneo yaliyokusudiwa au inaiachia Mikoa husika iamue yenyewe inavyoona inafaa?

(c) Je, Wilaya zinashirikishwa vipi katika kupanga barabara zinazostahili kushughulikiwa kila mwaka kutokana na fedha hizo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mbunge wa Gairo, naomba kutoa maelezo ya jumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sheria Na. 2 ya mwaka 1998 iliyoanzisha Bodi ya sasa ya Mfuko wa Barabara pamoja na mfuko wenyewe, imeainisha pamoja na mambo mengine, aina ya barabara na Asasi zitakazonufaika na fedha za mfuko.

Katika sehemu ya pili, kifungu cha 4, kifungu kidogo cha 3, sheria inabainisha kwamba asilimia 90 ya fedha za mfuko zitatumika kwa ajili ya matengezo ya kawaida na ya dharura kwa barabara zilizoainishwa kisheria pamoja na gharama za uendeshaji kulingana na mipango iliyoidhinishwa kwa maana ya barabara kuu na za Mikoa chini ya Wizara ya Ujenzi na Barabara za Wilaya na Miji chini ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kulingana na Bajeti zitakazopitishwa na Bunge.

Aidha, kifungu kidogo cha 4 kinasema kwamba kiasi kisichozidi asilimia 10 kitatumika kwa ajili ya kazi za maendeleo ya barabara pamoja na gharama za uendeshaji kwa Tanzania Bara na kama zilivyopitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, kifungu kidogo cha tano, kinasisitiza kwamba fedha hizi hazitatumika kwa shughuli nyingine yoyote, zaidi ya hizo zilizotajwa.

Kifungu cha sita kinampa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, mamlaka ya kukagua mahesabu na matumizi ya fedha za mfuko. Sehemu ya tatu ya sheria hii kifungu cha tano, vifungu vidogo vya 4 (h) na 4 (i) vinaipa Bodi ya Mfuko wa Barabara mamlaka ya kuhakikisha kwamba fedha za mfuko zinatumika vizuri na kulingana na madhumni ya mfuko.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kupitia sheria namba 2 ya mwaka 1998, Serikali imeweka taratibu wa kuainisha barabara zinazostahili kupatiwa fedha kila mwaka. Barabara zilizoanishwa kisheria *(classified)* ni Barabara Kuu, Barabara za Mikoa za Wilaya na za Miji. Mipango ya kila mwaka hutayarishwa na Wizara husika na kupitishwa na Bunge hili.

Baada ya kupitishwa na Bunge, Bodi ya Mfuko wa Barabara huingia mikataba ya utendaji na Wizara/Asasi husika za utekelezaji katika mikataba hiyo barabara husika na mipango ya kazi huainishwa. Aidha, barabara zilizo katika hali nzuri na hasa za lami ambazo zimejengwa kwa gharama kubwa zinapewa kipaumbele katika mipango ya matengenezo.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kupitia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, Bodi ya Mfuko wa Barabara inafuatilia matumizi ya Fedha za Mfuko ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba barabara zinazohudumiwa na aina ya kazi ni kama zilivyopitishwa na Bunge na kuainishwa kwenye mikataba ya utendaji.

Bodi ya Mfuko wa Barabara kwa kushirikiana na Wahandisi wa Mikoa na wale wa TAMISEMI, hufuatilia pia matumizi ya fedha hizo. Aidha, Waheshimiwa Wabunge waligawiwa Ripoti ya mwaka 2001/2002 ya Mfuko wa Barabara ambayo ilielezea pia ripoti ya ukaguzi wa fedha ya mfuko kwa watumiaji. Aidha, Bodi ya Mfuko wa Barabara

huajiri mshauri mtaalam *(Consultant)* kufanya ukaguzi wa kazi *(Technical Auditing)* kila mwaka.

Wizara/Asasi zinazopokea fedha za Mfuko wa Barabara hutengeneza taarifa ya utekelezaji ya kila robo ya mwaka na kuwasilisha kwenye Bodi ya Mfuko wa Barabara. Wizara/Asasi ambayo haileti taarifa ya utekelezaji haipelekewi fedha zingine mpaka taarifa iwasilishwe kwa Bodi ya Mfuko wa Barabara.

(c) Mheshimiwa Spika, Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji zimepewa mamlaka ya kuchagua na kupanga barabara na aina ya matengenezo yanayotakiwa kwa kuwahusisha Madiwani katika mabaraza yao. Mipango hii hupitishwa katika mabaraza kwa kufuata taratibu za Bajeti za mwaka kulingana na kiwango cha fedha kinachoelekezwa na bodi.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amefafanua vifungu vya sheria na jinsi hela zinavyopatikana na kwa kuwa amesema ziko hela zinazotengwa kupitia Bajeti inavyoletwa hapa Bungeni. Nilitaka kujua tu kwa sababu swali ni la ujumla, zile fedha za *STABEX* za kahawa zilizotengwa kwenda kujenga barabara zimejenga barabara kwenye Wilaya ngapi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Hilo nalo ni swali jipya lakini kama Waziri una majibu jibu, inaelekea unayo endelea.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, kama ifuatavyo:-

Fedha za *STABEX* hazihusiki kabisa na matumizi ya Wizara ya Ujenzi ama siyo zingepitishwa hapa kwenye Bunge na ninyi mngeziona. *(Makofi)*

**MHE. CAPT. THEODOS KASAPIRA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba fedha za *ADB* ambazo zinakuja kwa ajili ya ujenzi wa barabara zinapita kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii, badala ya kupita kwenye Wizara ya Ujenzi na Mikoa haijui? Kule Mahenge tuna matatizo na Wizara ya Maliasili na Utalii?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa *Captain* Theodos Kasapira, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii, inapata fedha za kutengeneza barabara katika sehemu zake za *National Park* ambayo hata mimi bahati nzuri nahusika kwa sababu *National Park* ninayohusika nayo na Mheshimiwa Kasapira ndiyo hiyo hiyo,

*Selous National Game Reserve* na mimi nimepata fedha hizo. Tatizo ni *design* ya barabara hizo. *Design* ya barabara ya hizo siyo barabara za kupita magari makubwa ni *four wheel drive design.* Inapangwa kwa sababu ya Watalii na wawindaji tu. Kwa hiyo, ni misaada inayopatikana kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii na utaratibu wake ni tofauti kabisa na hizi za Serikali.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona ili unipe nafasi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wilaya ya Mafia ni moja ya Wilaya ambayo inapokea fedha kutoka Mfuko wa Barabara wa Taifa na pia kupitia kitengo chake cha *TANROAD* kupitia Meneja wake wa Mkoa.

Swali langu ni kwamba kwa kuwa Mafia kuna tatizo kubwa sana la upatikanaji wa wakandarasi ambao wanakataa kwenda kufanya kazi za ujenzi wa barabara kutokana na kiwango kidogo cha pesa kinachotolewa na ama Mfuko wa Barabara au *TANROAD* kuja Wilayani Mafia. Sasa basi hivi juzi tumepata zaidi ya shilingi milioni 40, nilikuwa namwomba, Mheshimiwa Waziri kwa kuwa hizi ni pesa ni pesa ambazo zinatoka miongoni mwa walipa kodi wa nchi hii, anaweza kufunga safari kuja Mafia tena namwomba akifuatana na Kamati yake ya Miundombinu aje kuangalia jinsi mkandarasi alivyokuja kula pesa za Serikali ambazo hazikufanya jambo lolote na wakati huu inawezekana kabisa pesa hii, barabara zikaangamia kabisa, ili kuweza kuokoa pesa hizi za Serikali jamani? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdulkarim Shah, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimekubali tutapanga na Kamati tutakuja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, kabla hatujaendelea niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba kipindi hiki cha maswali ni wakati muafaka wa kuleta maombi ya kuchangia kwenye Miswada inayoonekana kwenye *Order Paper* ya leo. Maswali kwa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi Mheshimiwa Ali Said Salim.

Na. 5

**Fidia kwa Ardhi/Nyumba Zilizovunjwa**

**MHE. ALI SAID SALIM** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imekuwa ikiwalipa fidia wananchi wanaochukuliwa ardhi yao au kuvunjiwa nyumba zao kwa sababu mbalimbali.

Je, kwa nini hadi leo wananchi wa eneo la Kipawa karibu na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Dar es Salaam hawajalipwa fidia zao?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziwani, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba hadi sasa Serikali haijawalipa fidia wananchi wanaoishi kandokando ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Dar es Salaam.

Napenda nimjulishe Mheshimiwa Mbunge, kwamba uthamini wa fidia kwa wananchi waliojenga kandokando ya Kiwanja cha Ndege cha Dar es Salaam kwenye vitongoji vya Kipawa, Kigilagila na Kipunguni ulifanyika Septemba 1997. Uthamini huo ulibainisha kuwa gharama yote ya fidia ni kiasi cha shilingi bilioni 23, kiwango ambacho ni kikubwa kwa Serikali kuweza kulipa kwa mara moja. Katika kipindi chote hicho, Serikali imekuwa inatafuta fedha ili kuweza kuwalipa wananchi stahili yao. Katika mazingira ya sasa ya hali mbaya ya mvua katika baadhi ya maeneo nchini, matumizi ya Serikali yanaelekezwa katika upatikanaji wa chakula.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutafuta fedha kwa ajili ya fidia vile vile Serikali inapitia upya uthamini uliofanywa kuhakikisha kuwa unaendana na mazingira ya sasa ikilinganishwa na wakati huo. Pia napenda niwaarifu rasmi kuwa msimamo wa Serikali kwa wale waliojenga katika *road reserve,* uko pale pale kwamba hakutakuwa na fidia.

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu pamoja na wananchi kwa ujumla kuwa nia ya Serikali ya kukipanua Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Dar es Salaam ili kuweza kumudu ushindani wa biashara ya safari za anga na kuongeza Pato la Taifa bado ipo pale pale.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Mimi niko *concern* na hawa waliojenga kwenye *road reserve,* waliojenga kwenye *road reserve* kuna wengine walijenga kabla hata barabara yenyewe haijawekwa. Ni kwa nini Serikali ione kwamba hawahitaji fidia wakati huo sheria ilikuwa haijapitishwa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (k.n.y WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kabisa zipo nyumba ambazo zilikuwepo miaka mingi pengine kabla ya barabara. Lakini vile vile ni ukweli kwamba kila kitu kina wakati wake. Sasa hivi tumeamua kuzitambulisha nyumba zote ambazo zipo kwenye *road reserve* na tumezitilia alama ya *X* endapo tutapata fedha na kupitisha hapo tutamwambia huyo bwana kama anayo hati halali hiki naomba kieleweke  kama anayo hati halali anastahili kulipwa tutazungumza naye. Lakini kama hana hati halali maana yake Serikali inapitisha maendeleo hapo bila malipo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali huwa inaelewa mapema pale ambapo inataka kufanya miradi ya maendeleo na kwa kuwa wananchi wengi huvunjiwa maeneo yao ambapo Serikali inataka kufanya maendeleo na kuchukua miaka mingi Serikali kutokufanya yale maendeleo kwa mfano huo Uwanja wa Ndege watu wamevunjiwa zaidi ya miaka kumi hivi sasa na hawajapata fidia.

Kwa nini Serikali wakati haina fedha za maendeleo inaharakisha kuwavunjia watu nyumba wakati fedha za maendeleo yenyewe hazijapatikana, hawaoni kama wanatoa usumbufu kwa wananchi usio na sababu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (k.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali haionei watu katika kuweka alama ama kuvunja nyumba, inawatahadharisha, inawalipa kama ni lazima kuwalipa na inavunja na halafu wakati programu ya Serikali inaendelea watu huona kama Serikali vile imesahau lakini si kweli kwamba inawaonea kwa kuvunja halafu hawafanyi kitu. Inapokuwa tayari kufanya kitu itakuwa imefanya kitu wakati hakuna bughudha. Afadhali kuwaondoa sasa hivi wakati mipango ya Serikali huku inaendelea. Lakini wakati wote kuna nia na mipango sahihi ya Serikali ipo tayari. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hii ni nafasi ya maswali kwa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, kwa hiyo, naomba turudi kwenye Wizara inayohusika.

Na. 6

**Gharama za Simu kuwa Kubwa**

**MHE. RUTH B. MSAFIRI** aliuliza:-

Kwa kuwa mawasiliano ya simu ni mojawapo ya miundombinu ya msingi katika nchi yetu kiuchumi na kwa kuwa kampuni nyingi za simu hasa simu zisizo na waya zimeonyesha juhudi ya kufikisha mawasiliano hadi vijijini na kwa kuwa wananchi wamefurahia na wanapenda kutumia simu hizo kwa mawasiliano mbalimbali:-

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba gharama ya uendeshaji ni kubwa mno na inadhoofisha kusudio la kuwepo simu hadi vijijini kwani wananchi wana kipato kidogo?

(b) Je, kwa nini upigaji simu kwa kampuni yenyewe usiwe na gharama ndogo zaidi ya hivi ilivyo na kwa nini utumaji wa ujumbe *(message)* kwenye simu iliyo na fedha kwa kampuni ile ile isiwe bure na mtumiaji akatozwa kwa kampuni tofauti?

(c) Je, lini zitatumika thamani ya shilingi ya Tanzania kwa simu zote badala ya dola za Kimarekani?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa napenda nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba gharama za simu hapa nchini bado ni kubwa hasa kwa wateja wenye kipato kidogo. Kwa kuona tatizo hili Serikali kupitia Tume ya Mawasiliano ikishirikiana na Kampuni ya *ANALYSIS* ya Uingereza imefanya utafiti wa kutathmini gharama za ufungaji na uendeshaji mitambo ya simu *(cost based structure)* hapa nchini kwa madhumuni ya kujua bei halisi za simu ambazo wateja wa simu wanatakiwa kutozwa ikiwa ni pamoja na huduma ya ziada kama ile ya kutuma ujumbe *(message)* na kadhalika. Utafiti huu utawezesha kujua bei ya upigaji simu ndani ya mtandao husika na bei ya upigaji simu kutoka mtandao mmoja kwenda mtandao mwingine.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukweli kwamba watoa huduma za simu hununua mitambo yao kwa Dola za Kimarekani na kubadilika kwa thamani ya shilingi ya Tanzania mara kwa mara makampuni yote ya simu hapo awali yalikuwa yakitoza bei zake kwa ldola za Kimarekani. Lakini sasa kutokana na kilio cha wananchi, Serikali imeyashauri makampuni ya simu za mkononi yaanze kutoza gharama kwa shilingi. Hadi sasa makampuni ya *Mobitel, Celtel* na *Vodacom* yanatoza gharama zake kwa shilingi. Serikali itaendelea kuishauri *Zantel* nayo ianze kutoza gharama zake kwa shilingi.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

**SPIKA:** Hatukusikii, hebu uwe karibu na kipaza sauti.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Nakubaliana katika jibu la msingi imekubalika kwamba mawasiliano ni kitu muhimu kwa maendeleo na uchumi wa Taifa. Lakini kwa bahati mbaya moto tulioanza nao katika shughuli za mawasiliano hasa kwa simu unaanza kuzimika. *Call box* za *TTCL* sasa hivi hazifanyi kazi karibu nchi nzima. Walioanza kushabikia simu za mikononi pale zilipoanza sasa wanauza simu hizo kwa sababu ya gharama kubwa. Je, Mheshimiwa Waziri anasemaje kuhusu suala hili kama kweli nia yetu ni kuendeleza uchumi wa Taifa hili?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba moto wa maendeleo uko

pale pale ndiyo maana makampuni haya yamefika sehemu nyingi sana. Hata hivi karibuni mpaka Mpanda tumeshafika. Nia ni kuleta maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, simu za *TTCL* kama wanatoa wanafanya makosa lakini nafasi ipo ya kuendeleza sekta hii hasa kwa kutumia *Basic Telecommunication Services* na tunategemea tukimaliza muda wa huu, ushindani utakaokuwepo utaleta hamasa wa maendeleo ya simu kufika vijijini zaidi.

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri, atakubaliana na mimi kwamba gharama za simu zinaweza zikapungua kama makampuni haya yanayotoa huduma hizi wakishirikiana katika kutumia minara ya mawasiliano. Je, Serikali imefanya jitihada gani kuwashawishi watumie minara kwa pamoja?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba gharama zinaweza zikapungua pindipo wawekezaji wakikubali kushirikiana katika kutumia minara. Serikali kwa kupitia chombo kilichowekwa makusudi ku-*regulate* masuala haya ya simu kinafanya juhudi za kutosha na kuna sehemu nyingine wawekezaji wanakubaliana kushirikiana katika minara. Lakini niseme tu katika ushindani huwezi kumlazimisha, lazima atumie au ashee na mwenzake.

Na. 7

**Kutofautiana kwa Malipo ya Mafao kwa Watumishi Waliopunguzwa kazi**

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI (k.n.y. MHE. LUCAS L. SELELII)** alijibu:-

Kwa kuwa miaka ya 1990 hadi 1995 Serikali ilikuwa na zoezi la kupunguza kazi *(Retrenchment)* watumishi wa kada mbalimbali katika Mashirika na Idara za Serikali zilizo chini yake na Mashirika kama *NBC, UDA* na kadhalika:-

(a) Je, kwa nini malipo ya mafao yao yalitofautiaana kwa kila awamu yaani wale waliopunguzwa awamu ya kwanza walipata fedha kidogo kuliko awamu zilizofuata?

(b) Je, kwa nini hata malipo/mafao ya *PPF* nayo ni kidogo kuliko vyeo/wadhifa aliokuwa nao mtumishi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mbunge wa Nzega, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kumekuwepo tofauti ya malipo watumishi wa Serikali na Idara zake wanaopunguzwa kazini. Watumishi wa Serikali na Taasisi zake waliopunguzwa kazi, pamoja na malipo ya kisheria, walilipwa kama ifuatavyo:-

(i) Kwanza katika awamu ya kwanza walilipwa mkono wa heri mishahara ya miezi 40 kwa utumishi uiozidi miaka 10 kazini.

(ii) Katika awamu ya pili walilipwa mishahara ya miezi 20 kwa utumishi usiozidi miaka 10 kazini. Kupungua huko kunatokana na ukweli kwamba mishahara ya watumishi wa Serikali na Taasisi zake ilikuwa imeboreshwa kwa kiasi kikubwa.

Hata hivyo, zoezi la kupunguza watumishi wa Serikali na Idara zake lilifadhiliwa na wafadhili kupitia mradi wa Marekebisho Serikalini *(Civil Service Reform).*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa watumishi wa Mashirika ya Umma waliopunguzwa kazi, mafao yalilipwa kulingana na kwanza, Mikataba ya Hiari ya kila Shirika. Mikataba ya Hiari huwa na makubaliano tofauti kwa kila Shirika kulingana na uwezo wa kifedha. Pale ambapo hapakuwa na Mikataba ya Hiari, mafao ya kisheria *(Statutory Terminal Benefit)* yalilipwa.

(b) Mheshimiwa Spika, kulingana na sheria ya *PPF* wanachama wake hawapishani kwa vyeo. Mafao ya *PPF* yanalipwa kwa kuzingatia vigezo vitatu vifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, mshahara wa mwanachama ambao ulitumika kuwasilisha michango yake *PPF,* pili, muda wa uanachama ambao ni miezi aliyochangia na tatu, kanuni ya Pensheni iliyotumika wakati wa kukokotoa mafao ya mwanachama *(Pension factor).*

Mheshimiwa Spika, vigezo hivi vitatu ndivyo vinatoa kiasi ambacho mwanachama analipwa kama mafao yaani mkupuo na mafao ya kila mwezi au kiinua mgongo kwa wale wanaostahili.

Na. 8

**Noti Mpya**

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 2002/2003 Serikali ilichukua uamuzi wa kubadili fedha zake zoezi ambalo linasemekana liligharimu milioni nyingi za fedha na kwa kuwa lengo la kudhibiti noti bandia halijafanikiwa kutokana na matukio mengi yanayotolewa taarifa na vyombo mbalimbali vya habari kuhusu kuzagaa ovyo kwa fedha bandia.

(a) Je, fedha hizo zilitengenezwa na kampuni gani na ya nchi gani na je, kampuni hiyo imewahi kutengeneza fedha za nchi zipi?

(b) Kwa kuwa taratibu za matumizi ya fedha za Serikali zipo wazi kuhusu zabuni, je, ni kampuni ngapi zilizoleta maombi ya kutengeneza noti hizo na matangazo hayo yalitolewa katika vyombo vipi vya habari vya hapa ndani na vya nje ya nchi?

(c) Kwa kuwa fedha hizo mpya zilisemekana kwamba ni imara na pia ingekuwa vigumu kutengenezwa ovyo mitaani. Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu kuzagaa kwa noti bandia nchini katika muda mfupi baada ya noti mpya kuanza kutumika?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahimu Wankanga Marwa, Mbunge wa Musoma Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, noti zinazotumika Tanzania zinatengenezwa na kampuni ya Kijerumani iitwayo *Giesecke & Devrient Gmbh* au kwa kifupi *G & D.* Kampuni hiyo ni moja kati ya makampuni matatu makubwa zaidi duniani ya kutengeneza noti. Aidha, inao uzoefu zaidi ambao unafika miaka 150 katika kuchapa noti na nyaraka mbalimbali za kiusalama yaani *security documents and items.* Serikali ya Tanzania ilianza kutengeneza noti zake na kampuni hiyo mwaka 1996 kwa mara ya kwanza, kabla ya hapo noti zetu zilikuwa zinatengenezwa na kampuni ya *Thomas de la Rue* ya Uingereza.

(b) Mheshimiwa Spika, utengenezaji wa fedha za nchi yoyote ile, noti na sarafu, ni jambo nyeti na linahitaji usiri mkubwa ili kuhakikisha kwamba kunakuwa na usalama wa kutosha. Serikali ya Tanzania, kwa kutumia uzoefu wake, inayo majina ya makampuni makubwa ya Kimataifa yanayoongoza duniani katika utengenezaji wa fedha (noti na sarafu) yenye uzoefu wa muda mrefu na uadilifu wa hali ya juu.

Hivyo, kwa kuwa kazi ya kuchapisha noti ni nyeti na kwa kuwa makampuni ya kuchapisha noti ulimwenguni ni machache sana na yote yanajulikana, utaratibu unaotumika na Mataifa yote, pamoja na Tanzania, ni wa *closed tender* yaani ni kuyafahamisha makampuni hayo kuleta maombi yao, kwa mujibu wa taratibu zinazojulikana.

Mheshimiwa Spika, kulingana na utaratibu wa kawaida, safari hii pia Serikali ya Tanzania, ilizikaribisha kampuni hizo kubwa kushiriki kuomba zabuni ya kutengeneza toleo jipya la noti zetu. Makampuni yaliyoalikwa kuleta *tender* ni:-

1. *Thomas de la Rue* ya Uingereza
2. *Giesecke & Devrient Gmbh* ya Ujerumani

3. *Francois Charles Oberthur* ya Ufaransa
4. *Canadian Bank Note Company Limited* ya Canada

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema wakati najibu swali Na. 4 katika Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge lako Tukufu, utengenezaji wa noti bandia ni kitendo cha uhalifu, sawa na uhalifu mwingine kama vile mauaji, uporaji au wizi. Lakini hata hivyo, haina maana jitihada zisifanyike kudhibiti tatizo hili.

Kwa upande wetu Tanzania, tumejitahidi sana kudhibiti tatizo hilo. Njia ya uhakika ya kudhibiti kughushi inaanzia na raia mwenyewe. Noti zinazodhibiti ughushaji ni noti ambazo zinamwezesha raia atambue na kutofautisha kwa wepesi kati ya noti halali na noti bandia kwa kuitazama kila noti kwa makini kuona kama kweli ina alama zote za usalama ambazo Benki Kuu imezieleza kwa makini na kwa kirefu. Kwani mhalifu anayetaka kugushi akiona noti zake bandia zinakataliwa na kila mtu anashindwa kuzitia katika mzunguko ndipo atakapo kata tamaa na kuacha kugushi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutumia vyombo vyake vya dola inaendelea kulishughulikia suala la noti bandia. Wananchi pia wanaombwa wazidi kushirikiana na vyombo vya dola katika kutoa taarifa zozote zitakazosaidia kuwakamata wahalifu wanaojihusisha na utengenezaji wa noti bandia.

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa sababu zilizopelekea Serikali kupitia Benki Kuu kubadilisha mzabuni aliyetengeneza fedha mara ya kwanza ni kudhibiti ubora wa hizo noti na labda pengine kupata unafuu katika utengenezaji wa noti hizo. Lakini kwa kuwa bado tatizo hili la kugushi hizi fedha zipo, na kwa kuwa Jeshi la Polisi kwa kweli inafanya kazi nzuri sana.

Je, Waziri anawashirikisha vipi viongozi wa Jeshi la Polisi kuhakikisha kwamba unawekwa mkakati wa kuzuia tatizo hilo ambalo sasa linazidi kuwa kubwa kwenye nchi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Waziri anaweza kulieleza Bunge lako Tukufu sababu kuu za msingi ambazo zilisababisha tubadilishe hizo fedha za awali ambazo inaonekana zilikuwa hazifojiki kama hizi za sasa hivi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, sababu zilizoweza kubadilisha ni kwamba vigezo vyote viliwekwa kwa wale walioleta zabuni, aliyechaguliwa ndiyo aliyefuzu na alikuwa na yale mambo muhimu, alama ambazo zingeonyesha kujulikana haraka kwa hizi noti bandia.

Katika noti zilizokwisha kusanywa na Benki Kuu mara hii za sasa hivi ukilinganisha ni chache zaidi na Benki Kuu wanapotoa noti mpya mara zote huwa wanatangaza alama zilizomo katika noti zile ili wananchi wazijue, noti ya elfu kumi au shilingi elfu tano au yoyote ile ina alama gani za muhimu kujua kama ni kweli na eti

kwamba noti zinagundulika haraka hiyo ina maana kwamba alama zake zinaonekana kwa haraka.

Kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba hawa waghushaji wa noti hawa ni wahalifu na bila shaka katika alama za ndani na wanaangalia kwamba mwananchi wa kawaida hawezi kuangalia kwa undani kabisa ile noti yake kwamba amepewa noti kwamba ina alama zile na ndiyo maana anatumia kwa haraka.

Lakini kwamba zinaonekana kwa haraka ina maana basi alama zake ni sahihi zaidi kwa hivyo, *BOT* au Serikali haikukosea katika kuchagua mzabuni yule na kwa takwimu zetu ni noti chache zaidi ambazo ziko *Bank of Tanzania* ambazo zimeghushiwa kuliko ilivyokuwa hapo mwanzo.

Uhusiano wa Polisi bila shaka, Polisi wanatumika na Polisi si lazima kwamba *BOT*. Polisi nao ni wananchi, nao katika ufahamishaji wa aina ya alama mbalimbali za noti zile bila shaka nao ni wale wa mwanzo kujizujua na wale wanashirikiana kabisa kuhakikisha kwamba noti zile wanazishika waweze kusema kwamba hii kweli haijakamilika katika alama zake na kwa hivyo ni noti ambayo imegushiwa kabisa.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa sarafu ya shilingi 100 inaonekana ubora wake ni mbovu sana na kwamba imekataliwa kupokelewa. Je, Wizara, Serikali imechukua hatua gani za kurekebisha mapungufu haya?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, *BOT* inavyofahamu Serikali imepata malalamiko juu ya hii sarafu ya shilingi 100 na inalifanyia kazi.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Watanzania sisi tuliokuwa tunataka ni noti mpya, lakini Benki Kuu wakaenda mpaka kiwango cha kuonyesha jinsi hizo noti zinavyotengenezwa. Je, hawajui kwamba hiyo ilikuwa inatoa mwanya kwa watu wanaoweza kughushi na mtindo huu uachwe usirudiwe tena?

**SPIKA:** Waziri hakuelewa swali, naruhusu ulirudie.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, naomba nirudie swali langu kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa wakati Benki Kuu inatangaza juu hizi noti mpya walikuwa wanaonyesha hata zile mashine zinazotengeneza hatua kwa hatua kitu ambacho kingewapa mwanya hata hawa wanaogushi kujua jinsi ya kutengeneza hizo noti. Serikali haioni kwamba kitendo hicho kinawafundisha hawa wanaogushi na kisirudiwe tena?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, Benki Kuu huwa inaonyesha mfano tu, kwa sababu hata wao Benki Kuu hawana hizo aina ya mashine zinazotengeneza noti. Kwa hiyo, watu hao waghushaji hao wanachotumia ni *simple technology* ambayo zile alama za undani sasa kwa *simple photocopying* kugeuza huku na huku haiwezi ikazifanya.

Kwa hiyo, kama nilivyosema, ukiangalia noti za *dollar* na noti za *Euro* na *Japanise Yen* vile vile zinagushiwa sana na katika taarifa za fedha utakuta kwamba matatizo hayo bado yapo na hata kama wanagushi lakini bado zinashikwa.

Na. 9

**Mipaka ya Tanzania**

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza:-

(a) Je, Mipaka ya Tanganyika na baadaye Tanzania kwa mara ya kwanza iliamuliwa na nani na ni kigezo kipi kilitumika kuamua juu ya Mipaka?

(b) Je, Mpaka wetu katika Ziwa Nyasa mbona haujulikani kwa sababu kila ramani ina mpaka tofauti?

(c) Je, wananchi wanaoishi Mipakani kwa makosa ya kutojua Mipaka yao, Serikali huwashughulikiaje?

**SPIKA:** Bunge halina Mwenyekiti. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mipaka kati ya Tanganyika na baadaye Tanzania na nchi jirani iliwekwa kwa protokali kati ya wakoloni waliokuwa wanazitawala nchi hizo. Kamisheni ya Upimaji wa Mipaka kati ya nchi yetu na nchi jirani ilifanyika mwaka 1909 ambayo ilijumuisha utawala wa Uingereza, Ujerumani na Ubeligiji. Kigezo cha protokali hizo ni Mipaka waliyokubaliana kuwa ndiyo maeneo ya Utawala wa Makoloni yao, hakuna kigezo kingine.

(b) Mheshimiwa Spika, Tanzania inafahamu kuwa mpaka wake katika Ziwa Nyasa kwenye mpaka kati ya Tanzania na Malawi uko katikati ya Ziwa Nyasa kuanzia mdomo wa Mto Songwe. Baadhi ya ramani zimekosewa, ambapo zimechorwa na kuonyesha kuwa mpaka unapita katika kingo za Ziwa kwa upande wa Tanzania. Makosa yoyote katika ramani yanategemea mtengenezaji na jinsi alivyoelewa vigezo muhimu

katika kuweka mpaka kwenye maeneo ya maji kama ya Ziwa Nyasa. Kutokana na dosari hizo, Wizara yangu kama msimamizi Mkuu wa ramani nchini imewaandikia barua wote wenye kutoa ramani zenye makosa kufanya marekebisho au kutumia ramani sahihi kutoka Serikalini.

(c) Mheshimiwa Spika, Halmashauri zote za Wilaya zinazopakana na nchi jirani zinawajibika kufahamu Mipaka yake. Tatizo la kutofahamu Mipaka linaendelea kupanuka kutokana na alama za Mipaka ama kung'olewa au Mpaka kutofyekwa kwa muda mrefu. Ni wajibu wa Halmashauri za Wilaya kwa kushirikiana na Wilaya za nchi jirani kulinda alama za Mipaka isiharibiwe na kuhakikisha Mipaka imefyekwa na kuwa wazi wakati wote ili wananchi wa pande zote watambue mapito ya Mipaka ya Wilaya zao.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa wananchi wanaoishi karibu na Mipaka ya nchi jirani kuwa kwanza, mamlaka husika zijenge ujirani mwema, pili, washirikiane na Halmashauri za Wilaya kufyeka Mipaka mara kwa mara na kuweka wazi njia za mapito ya Mipaka na tatu Halmashauri za Wilaya kwa kushirikiana na mamlaka zinazohusika, zitambue wananchi wake wanaoishi nje ya Mipaka na kuwarejesha ndani ya Mipaka ya nchi zao.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba radhi nimetoka juzi kwenye Mikutano ya Kimataifa na wenyeviti ndiyo tuliyokuwa tunawatumia.

Ningeomba sasa niulize maswali mawili ya nyongoza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, je, Waziri atakubaliana nami ya kwamba kwa uhusiano wetu ambao ameujenga Mheshimiwa Rais wetu Benjamin William Mkapa na nchi jirani zote ni nzuri kwa kipindi hiki na kwa kuwa wakati wowote baadhi ya viongozi hawa watakuwa wanang'atuka katika uongozi.

Je, si wakati muafaka hili suala zima la mipaka hasa katika sehemu ambayo ameitaja Mheshimiwa Naibu Waziri wakalikamilisha kabla ya kipindi cha Mheshimiwa Rais kumaliza muda wake?

La pili, je Waziri anajua ya kwamba Mipaka iliyopo katika Maziwa ya Victoria Ziwa Tanganyika, Ziwa Jipe, Ziwa Nyasa haijulikani kwa wavuvi na wavuvi wamekuwa ni tatizo kupigana kutokana upande mmoja hadi upande mwingine kwa kuwa Mipaka yenyewe haijulikani rasmi?

Je, Waziri asingefanya mpango wa kuwa na doria, kuwa na vyombo vya doria ili wananchi nao wakajulishwa mipaka ni ipi katika ziwa ili wasiwe wanavamia upande mwingine?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli uhusiano wa majina na nchi yetu ni nzuri. Lakini bila watendaji kutusaidia kazi hizi kutambua maeneo, kufanya kazi ya ziada katika upimaji, hata marais wakakaa mara ngapi wakaiona vizuri kazi kutekelezeka. Kwa hiyo,

Mheshimiwa Mbunge tuendelee kuvuta subira ili kazi hiyo watalaam tuliyowaachia waendelee kufanya.

Kwa mfano sasa hivi, katika Ziwa Nyasa Mpaka wa Ziwa Nyasa utashughulikiwa vizuri baada ya Mpaka wa Mto Songwe kukamilika kazi zake. Tumeanza na tayari wameshatiliana mikataba. Kwa hiyo, Mto Songwe ukishashughulikiwa ambao unaleta maji mengi katika Ziwa Nyasa basi mara moja kazi ya mpaka wa Ziwa Nyasa utashughulikiwa. Hapa ni utaalam siyo siasa.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge kufanya subira hata Malawi nao wana uchaguzi mwaka huu. Kwa hiyo, tukisema kwamba tumalize uchaguzi tuanze na sisi mwakani tunafanya uchaguzi. Lakini haya ni mambo ya kiutendaji, naomba Mheshimiwa Mbunge, nakuhakikishia kwamba kazi itafanyika. Mpaka ulio katika maziwa ambao wavuvi hawaufahamu si rahisi wavuvi kufahamu. Inataka mtu mwenye kuelewa mtu mwenye ujuzi na kutumia dhana si rahisi kila nchi ikawa dhana kwa ajili ya kufanya doria katika maziwa au katika mito. Iliyobaki ni sisi wenyewe tu na wananchi wetu tuendelee kuwaelimisha ndugu zetu kwamba mvue angalau mfike mahali ambapo wasiingie katika *deep sea* itawahatarishia kwanza maisha yao, halafu pili kuhatarisha kwenda katika nchi ya jirani. Lakini pindi nafasi ya Serikali itakapokuwa ina uwezo wa kuweka doria hili jambo litafanyika.

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ninalo swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa haya mawe ya Mipakani yamechimbiwa kwa umbali mrefu sana kiasi kwamba wananchi hawawezi kujua huu ndiyo Mpaka au siyo na kwamba wanajikuta wamelima au kufuga au kuendeleza maisha yao nje ya mipaka ile. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kusimamia zoezi hili la kuweka mawe ya Mipaka karibu karibu japo mita mia tano, mia tano, ili wananchi hao waweze kujua mipaka yao na wasiingiliane Mipaka kwa Mipaka hivyo kuhatarisha vita vya Mipakani?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli nakubaliana naye kwamba mawe yakiwa mbalimbali sana si rahisi wananchi kuweza kutambua mpaka wao upo wapi. Serikali imeanza jitihada hizo mpaka wa Uganda ambako hata viongozi walilima mashamba mpaka ndani ya Tanzania. Hata Kenya hali kadhalika, lakini tumeanza kazi hiyo kuweza kufyeka halafu pili kusogeza angalao mawe kidogo, lakini ni gharama. Kwa hiyo, twende taratibu na fedha tulizo nazo lakini pia na wananchi kama nilivyosema katika jibu la msingi tuwaelimishe wananchi wetu wasiende katika maeneo ambayo hayawahusu na Halmashauri pia zisaidie na sisi wenyewe Wabunge tuendelee kuhamasisha ambao tuko katika majimbo ya mpakani.

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa katika jibu lake la msingi Mheshimiwa Waziri amesema ameziweka Halmashauri za Wilaya kutunza Mipaka ile pamoja na kufyeka ili alama ziweze

kuonekana. Nilitaka tu kujua kama Serikali inazisaidia Bajeti Halmashauri zilizo katika Mipaka ili kuziwezesha kutunza Mipaka hiyo kufyekea na hata kuonyesha mawe yalipo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, si rahisi kutoa pesa kwenye Wizara kusaidia Halmashauri. Kwanza matatizo yanayojitokeza kwa wananchi ni Halmashauri zenyewe ambazo nimesema kwamba zisaidie kwa sababu Serikali ni moja. Kwanza zisaidie kutokuleta ugomvi kati ya Wilaya na Wilaya au Wilaya na Wilaya ya nchi nyingine kwa kuwasaidia wananchi wetu, pia na sisi tutambue mipaka yetu.

Lakini pindi ambapo tunapata pesa za kutosha sisi ndio tunaohangaika pia kuweza kuonyesha ile mipaka kama nilivyosema mpaka wa Uganda na Kenya tumesaidia kama Wizara. Lakini bado tunasisitiza kwamba sisi peke yetu hatuwezi kumudu gharama hizo kwa hiyo Halmashauri nazo ni budi kuona uzito wa makazi ya wananchi na pia hatari ya usalama katika mipaka yao basi tuendelee kusaidiana ili tuhakikishe kwamba kila mtu anakaa sehemu yake na mipaka hii haingiliwi.

Na. 10

**Utoaji wa Hati za Nyumba na Mashamba**

**MHE. RAYNALD A. MROPE (k.n.y. MHE. OMAR M. MWENDA)** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wengi wanataka kukopa pembejeo za kilimo lakini masharti ya mikopo ni lazima mwenye kukopa apeleke Hati ya nyumba au shamba; na kwa kuwa wanaotoa Hatimiliki ni Makao Makuu ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi iliyoko Jijini Dar es Salaam ambako ni mbali na wananchi wengi wanashindwa kwenda huko kwa sababu ya uwezo wao mdogo na matatizo mengine mbalimbali:-

(a) Je, Serikali iko tayari kukasimu madaraka ya utoaji Hati za mashamba na nyumba Mikoani ili iwe rahisi kuwahudumia wananchi kwa karibu?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba wakati sasa umefika kwa kila mkulima apimiwe shamba lake na kupatiwa Hatimiliki?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omar Mohammed Mwenda, Mbunge wa Kilwa Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imekasimu madaraka ya uandaaji wa Hati za mashamba na viwanja katika Ofisi za Ardhi za Wilaya na Manispaa husika. Baada ya

kuandaliwa, Hati hizo huwasilishwa kwa Kamishna wa Ardhi kwa ajili ya mambo matatu. Jambo la kwanza, kuhakiki uandaaji wake ili kurekebisha kama itakuwa na makosa; jambo la pili, ni kuwekwa saini na Kamishna wa Ardhi na jambo la tatu, ni kuweka lakiri ya Kamishna wa Ardhi. Hati ni kumbukumbu muhimu sana hivyo inaandaliwa kwa makini ili isiwe na makosa.

Kama Hati iliyoandaliwa katika Wilaya na Manispaa haitakuwa na makosa na kurejeshwa kwa wahusika kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho, Hati zilizowasilishwa kwa Kamishna wa Ardhi kwa ajili ya saini na lakiri ya Ofisi yake hukamilika ndani ya siku kumi na nne (14) hivi sasa. Hati zilizokamilika hurejeshwa katika Ofisi ya Msajili wa Hati wa Kanda husika kwa ajili ya kusajiliwa na hatimaye mteja huichukulia huko.

Taratibu hizo zimewekwa kwa lengo la kuwa na nyaraka moja inayotambulika na kuzuia hatari ya kugushiwa.

Aidha, Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na.5 ya mwaka 1999, imeweka utaratibu wa Serikali za Vijiji kutoa Hatimiliki za kimila zenye hadhi sawa na hati miliki zinazotolewa na Ofisi ya Kamishna wa Ardhi.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge. Hata hivyo, kazi ya kupima shamba la kila mkulima inahitaji fedha nyingi. Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Jiji, Manispaa, Miji na Wilaya zitatekeleza jukumu hilo kulingana na upatikanaji wa fedha.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa mujibu wa Sera na Sheria za Ardhi, mwananchi binafsi anaweza kuomba kupimiwa eneo lake kupitia Ofisi za Ardhi Mikoani kwa kuchangia gharama kidogo tu za upimaji. Aidha, wananchi wanaweza kuwatumia wapimaji binafsi wanaotambuliwa kisheria kupima viwanja na mashamba yao.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa nini kusiwepo utaratibu wa hii mikopo itolewe moja kwa moja kwa wazalishaji, kwa mfano *SACCOS* badala ya kutegemea hizi Hati za nyumba na kadhalika?

(ii) Pembejeo za korosho huwa zinachelewa sana kila mwaka je, Serikali itathibitisha namna gani ubora wa kuleta hizi pembejeo kwa wakati ili kusaidia wakulima wa korosho?

**SPIKA:** Sidhani kama swali la pili linahusu Wizara hii, lakini la kwanza linaweza kujibiwa. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu Hati kupitia kwenye *NGOs, SACCOS* na kadhalika sio rahisi. Kama nilivyosema kwenye jibu la msingi lazima tudhibiti Hati hizi.

Mheshimiwa Spika, mambo ya kughushi ni mengi na ardhi ni kitu nyeti na ardhi iko chini ya Rais, kwa hiyo tutamtia aibu kwa kweli ikiwa hata Hati zinaweza kughushiwa. Sasa hivi tu tayari zinakughushiwa ingawa ziko *centrally* katika kuzitengeneza sasa tukiendelea kusema kila mmoja tumkabidhi mpaka tena *NGOs, SACCOS,* nafikiri tuendelee na utaratibu ule ule kwa sababu bado sasa hivi una uhakika wa kupata Hati haraka na mtu anaweza kuchukua akaenda kukopa anakokwenda kukopa.

Mheshimiwa Spika, swali la pembejeo za kilimo, naomba Waziri wa Kilimo na Chakula, aweze kuendelea kulijibu ipasavyo.

**SPIKA:** Hapana, hapana, Spika hajaruhusu lijibiwe na Waziri yeyote. Liletwe upya kwa sababu ni swali jipya kabisa. *(Kicheko)*

Na. 11

**Askari wa Usalama Barabarani**

**MHE. MUHAMMED RAJAB SOUD** aliuliza:-

Kwa kuwa baadhi ya Askari wa Usalama Barabarani *(TRAFFIC)* hawaelewi wajibu wao kuwa ni kuwaelimisha wanajamii kuhusu utumiaji wa barabara na kuweka mbele maslahi yao zaidi:-

(a) Je, Serikali itachukua hatua gani kuwaelimisha Askari hao?

(b) Je, tabia ya kujificha kwenye vichaka na kujitokeza ghafla barabarani, ni utendaji walioelekezwa au ni kusababisha ajali zisizo za lazima?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mbunge wa Jang'ombe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa baadhi ya Askari wachache wa usalama barabarani hawaelewi wajibu wao wa kuelimisha jamii kuhusu utumiaji wa barabara. Kwa sababu hiyo, kupitia Mabaraza ya Askari wa Usalama Barabarani, Askari hupewa maelekezo ya namna ya kutekeleza na kusimamia kazi za usalama barabarani pamoja na kuelimisha wanajamii kuhusu matumizi sahihi ya barabara. Mabaraza hayo pia hutumika kuwaasa Askari kufanya kazi zao kwa nidhamu kwa kuzingatia haki, sheria na kuacha kujihusisha na vitendo vyo vyote vinavyoliaibisha Jeshi la Polisi na kwa kuweka mbele maslahi binafsi.

Aidha, hivi karibuni Serikali imeanza kuendesha Mafunzo ya Msasa kwa Askari wote wa Usalama Barabarani. Mafunzo haya, tayari yametolewa kwa Askari wa Usalama Barabarani katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Iringa, Ruvuma na Mbeya. Mikoa mingine ni pamoja na Tanga, Kilimanjaro, Arusha na katika Mikoa yote mitano ya Tanzania Zanzibar. Lengo ni kutoa mafunzo haya kwa Mikoa yote hapa nchini ili kuwasaidia Askari kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

(b) Mheshimiwa Spika, mbinu ya Askari kujificha kwenye vichaka na kujitokeza ghafla barabarani ina lengo la kuwakamata madreva wa magari ya abiria ambao hukiuka Sheria za Barabarani. Kwa mfano kuendesha magari zaidi ya mwendo unaokubalika kisheria wa kilomita 80 kwa saa katika barabara kuu. Askari hulazimika kufanya hivyo ili kuwanasa madreva hao ambao hupeana ishara au kujulishana kwa redio mahali walipo Askari hao barabarani ili wapate fursa ya kuficha makosa yao.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hakuna taarifa yoyote iliyopokelewa ya kutokea kwa ajali barabarani iliyosababishwa na Askari hao kujificha na kujitokeza ghafla. Hata hivyo, Serikali inao mpango wa kuwawezesha Askari hawa kutumia mbinu za doria za kisasa za kuwanasa madreva wasiotii sheria za barabarani kama vile kuweka katika barabara kuu kamera za kuchunguza kasi ya mwendo wa magari, kufanya doria katika barabara kuu kwa kutumia magari au pikipiki. Uwezeshaji huu utatolewa hatua kwa hatua kutegemea kukua kwa uchumi wa Taifa letu na ongezeko la Bajeti ya Polisi.

**MHE. ANATORY K. CHOYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa hakuna utaratibu ambao unaeleweka ambao uko tayari kwa ajili ya kuwapa adhabu wale Madreva wanaosababisha ajali barabarani nikiwa na maana kwamba ajali zinapotokea barabarani kawaida Madreva huwa wanatoroka na Wizara haijaweka utaratibu maalum wa kuweza kuwanasa. Je, Wizara iko tayari kuweka utaratibu wa kuweka picha zao na maelezo yao katika magazeti mbalimbali pindi wanapopatikana waweze kuchukuliwa hatua ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa leseni zao za kuendesha?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli baadhi ya Madreva ikishatokea ajali hutoroka na sasa hivi kwa kweli Polisi wanatumia mbinu za kizamani tu za kutafuta kutegemea na taarifa za wananchi walioona tukio na mbinu mbalimbali. Lakini jinsi tunavyoendelea kama nilivyosema katika jibu langu la msingi katika barabara kuu tunatazamia kuweka *cameras* katika maeneo fulani fulani ambayo si tu kwamba zitatazama kasi ya mwendo lakini vile vile na matukio kama hayo, zitachukua gari, namba ya gari, saa ngapi na kadhalika. Kwa hiyo, kwa sasa hivi tunaomba tu wananchi popote pale walipo tuendelee kusaidiana na Polisi kuwanasa Madreva hawa kwa sababu inapotokea ajali Polisi hayupo pale. Kwa hiyo, kwa kweli tutategemea taarifa za raia wetu mpaka hapo ambapo tutapata dhana za kisasa.

Kuhusu kutoa matangazo ya picha ili wananchi wawatambue, hayo yanafanywa si katika ajali tu na katika matukio mbalimbali. Tunatoa shukrani kwamba baadhi ya watu mbalimbali wanatusaidia na tunaomba waendelee kutusaidia zaidi.

Na. 12

**Wafungwa wa Makosa Yanayohitaji Hukumu ya Kunyongwa**

**MHE. MONICA N. MBEGA (k.n.y. MHE. SALOME J. MBATIA)** aliuliza:-

Wakati akitoa hotuba yake, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Omar R. Mapuri (Mb), Bungeni akiwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2003/2004; Jedwali Na.10, uk.51 lilisomeka: "Wafungwa waliokuwepo Magerezani Tanzania Bara tarehe 1 Aprili, 2003 kuzingatia urefu wa vifungu vyao" lilionyesha kosa la Wafungwa wanaongojea kunyongwa ni, wanaume 359 na wanawake 11, sasa je:-

(a) Ni makosa ya aina gani hasa yaliwasibu Wafungwa hao hadi kupata hukumu hiyo?

(b) Nini maelezo ya kuwa Tanzania Wafungwa kama hawa huwa wanaishia kufungwa kifungo cha maisha kutokana na msamaha wa Rais (jambo ambalo ni jema) na ukweli kuwa hakuna aliye juu ya sheria; dhana hizi mbili hazigongani *(conflicting) i.e.* Mahakama kutoa adhabu ya kifo na Rais kuwa na uwezo wa kutoa msamaha?

(c) Ikizingatiwa wanawake kiuwiano na wanaume, wanawake ni wengi zaidi, je, Taifa linasemaje kuhusu utiifu wao wa sheria mbalimbali na hivyo kuwa wachache zaidi katika kupata adhabu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salome J. Mbatia (Viti Maalum) lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni ya Adhabu, ni makosa ya aina mbili tu ambayo adhabu ya kifo hutolewa. Makosa hayo ni ya mauaji ya kukusudia *(murder)* na kosa la uhaini *(treason).* Aidha, Wafungwa wanaume 359 na wanawake 11 waliokuwepo Magerezani tarehe 1 Aprili, 2003 wakingojea kutekelezwa adhabu ya kifo, aina ya makosa waliyoifanya ni mauaji ya kukusudia *(murder).*

(b) Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 vifungu vya 39, 196 na 197 vinawapa Majaji uwezo wa kutoa adhabu ya kifo kwa aina ya makosa yaliyotajwa; wakati huo huo Katiba ya Jamhuri ya Muungano Ibara ya 45(i)(c) imempa uwezo Mheshimiwa Rais wa kubadili adhabu ya kifo na kuwa ya kifungo Hali hii sio mgongano wa madaraka kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema bali ni mgawanyo wa

madaraka baina ya Mahakama *(Judiciary)* na Serikali *(Executive)* kwa mujibu wa Katiba wa Nchi ambayo ndiyo Sheria Mama.

(c) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002 idadi ya wanawake nchini ni wengi kuliko wanaume. Tarehe 1 Aprili, 2003 idadi ya wanawake waliofungwa wakingojea kunyongwa ilikuwa ndogo sana ukilinganisha na idadi ya wanaume. Takwimu hizi zinaonyesha wazi wazi kuwa wanawake ni watiifu zaidi wa sheria kuliko wanaume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitarudia kwa ruhusa yako, takwimu hizi zinaonyesha wazi wazi kuwa wanawake ni watiifu zaidi wa sheria kuliko wanaume na hivyo wanastahili kupongezwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ndiyo!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Nawaomba wanaume nao waige mfano huu mzuri wa wanawake. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Baada ya dhana nzima ya haki za binadamu kuingizwa katika Katiba ya nchi yetu je, hukumu ya kifo Tanzania bado ni halali?

**SPIKA:** Aah, hiyo ni, eeh, sawa Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli haki za binadamu zimeingia katika Katiba yetu ya nchi na Serikali yetu inafuata mfumo huo wa kuzingatia haki za binadamu lakini sheria ya kifo bado tunayo kwa sababu Watanzania wengi bado wanaamini kwamba wewe kumwua mwenzako kwa kukusudia vile vile umemnyima haki yake maana huyu uliyemwua huyu naye ana haki yake ya kibinadamu. Sasa wewe umeivunja wakitaka kukuua wewe ndio unasema kuna haki ya binadamu. Kwa hiyo, sheria hii bado ina mantiki, tutaendelea kuitumia mpaka hapo Watanzania walio wengi watakaposema kwamba tuiache. *(Kicheko)*

**MHE. PHILLIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Waziri anasema ni kweli kwamba sheria ya hukumu ya kifo bado ipo kwa ajili hiyo basi anataka kuliambia Bunge na Taifa kwamba sheria hiyo iko juu ya Katiba ya nchi ambayo ni Sheria Mama?

**SPIKA:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali, majibu!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (k.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI):** Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, ambayo inatambua haki za binadamu, miongoni mwa haki za binadamu ni haki ya kuishi.

Katiba hiyo hiyo katika Ibara ya 30 inaweka utaratibu unaoruhusu Waheshimiwa Wabunge kutunga sheria ambazo zitaweka taratibu kwa masuala ya haki za binadamu na Katiba hiyo hiyo ambayo ndio msingi ambao unaruhusu kuwepo kwa adhabu ya kifo. Kwa maana hiyo, hakuna mgongano wowote wa adhabu ya kifo kuendelea kutolewa na Mahakama zetu hapa nchini.

Na. 13

**Vikundi Vidogo Vidogo vya Ufundi**

**MHE. SEMINDU K. PAWA** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa vijiji vya Kibuko Mwarazi, Changa, Luholole, Kiroka, Bamba, Kiziwa, Mkulazi, Matuli, Maseyu, Kidugalo, Mikese, Mkuyuni, Kinole, Tegetero na Tununguo, wameunda vikundi vidogo vidogo vya ufundi 40 vya uzalishaji mali:-

Je, Serikali inawapa ushauri gani wananchi hao na wengine wa aina hiyo juu ya kupatiwa mikopo ya *SIDO?*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Semindu Pawa, Mbunge wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali, kwa kupitia Shirika lake la *SIDO,* hutoa huduma mbalimbali zinazolenga kumpa mwanga na kumsaidia mwananchi wa kawaida kupata uwezo wa kutatua matatizo yake mwenyewe hapo alipo. *SIDO* hutoa elimu ya biashara, mafunzo ya ufundi, ushauri wa mambo mbalimbali ya kiufundi na kibiashara, utoaji wa mitaji midogo ya kuanzisha au/na kuendeleza miradi ya uzalishaji mali. Hali kadhalika, *SIDO* inajishughulisha na uimarishaji wa vikundi.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka 2002/2003, *SIDO* iliandaa na kutoa mafunzo *(course)* 17 zilizojumuisha watu 340 za mafunzo ya elimu ya biashara na usindikaji wa vyakula na kutoa jumla ya mikopo 504 yenye thamani ya Sh.235.9 milioni katika Mkoa wa Morogoro.

Kwa vile mahitaji ya wananchi na hasa vikundi vya uzalishaji mali yanatofautiana kulingana na mazingira ya miradi husika, tunashauri vikundi na wananchi kwa ujumla walio katika hatua mbalimbali za uanzishaji na uendelezaji wa miradi ya uzalishaji mali na biashara, wawasiliane na Ofisi za *SIDO* za Mikoa yao ili ziweze kushauriana nao na hatimaye kupata namna inayofaa kuwahudumia. Aina ya huduma na hatua zitakazofuatia zitaamuliwa baada ya tathmini ya mahitaji halisi ya miradi kufanywa. Kwa kuzingatia maelezo hayo, namshauri Mheshimiwa Mbunge avishauri vijiji vya Kibuko Mwarazi, Changa, Luholole, Kiroka, Bamba, Kiziwa, Mkulazi, Matuli, Maseyu, Kidugalo, Mikese,

Mkuyuni, Kinole, Tegetero na Tununguo wawasiliane na Ofisi ya *SIDO* ya Mkoa wa Morogoro ili mahitaji ya vikundi hivyo yaweze kubainishwa na huduma mahsusi kwa ajili yao kutolewa.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza lenye sehemu (a) na (b). Kwanza tayari nimeshawasiliana na Mkoa wa Morogoro ndio maana nimekuja kuuliza swali hili hapa. Nimewasiliana na Mkoa na tumepata fomu za kujaza na tumejaza ziko Mkoani pale, kwa hiyo naomba atoe mwelekeo kwamba mikopo hiyo itolewe na sio hii, hii ni *sampling* tu. Viko vijiji vingi tu katika Mkoa huo, je, anakubali kuja kutembelea vikundi hivyo maeneo ya Ngerengere na Mkuyuni tu ili aone vikundi hivyo pamoja na kutoa hamasa kwa wanachama?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakubali kabisa kuja kutembelea vijiji vya Mikese na Mkuyuni au na vingine atakavyovitaja.

Pili, ningependa pia kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa mikakati ya *SIDO* tunayofanya sasa tunatoa mikopo kwa vikundi vyenye miradi ambayo inatekelezeka. Kwa hiyo, sasa hivi mchanganuo unafanyika, mafunzo yataendelea kutolewa na kama vitafuzu kupita na miradi ionekane inatekelezeka, nina hakika watapata mikopo.

Na. 14

***Lip Sticks***

**MHE. AISHA P. MAGINA** aliuliza:-

Kwa kuwa rangi za midomo wanazopaka akina mama zijulikanazo kama *Lip Sticks* mara nyingi huwa zinamezwa kupitia njia ya kujiramba mdomo:-

(a) Je, rangi hizo zinaweza kuwa na madhara gani tumboni?

(b) Je, Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* limewahi kufanya uchunguzi juu ya madhara ya rangi hizo?

(c) Je, rangi hizo zinaagizwa kutoka nchi gani na zinatengenezwa kwa kutumia nini?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Magina, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, rangi za midogo wanazopaka akina mama zijulikanazo kama *Lip Sticks* ambazo zimetengenezwa kwa kutumia rangi ambazo zimeorodheshwa katika kiwango husika haziwezi kuleta madhara yoyote tumboni. *(Makofi)*

(b) *TBS* kwa kutambua kwamba kuna rangi ambazo zinaweza kuleta madhara, inaandaa kiwango cha Kimataifa kinachoorodhesha rangi ambazo hazina madhara kwa watumiaji. Lakini kwa wakati huu, *TBS* kwa kutumia sheria yake ndogo ya viwango yaani *The Standards Compulsory Batch Certification of Imports Regulations 1998* na kwa kutumia viwango vilivyopo vya nchi nyingine, hupima ubora wa *Lip Sticks* kabla ya kuruhusiwa kuingizwa nchini Tanzania.

(c) Rangi za midomo huagizwa kutoka nchi mbalimbali duniani zikiwemo Afrika ya Kusini, nchi za Ulaya, nchi za Marekani, India na Mashariki ya Mbali. Kama nilivyoeleza hapo awali, *TBS* inahakiki ubora wa *Lip Sticks* hizo kabla ya kuruhusiwa kuingizwa nchini Tanzania.*Lips Sticks* hutengenezwa kwa kutumia rangi, *stearic acid, petroleum jelly* na nta.

**MHE. HAROUB S. MASOUD:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa ametoa maelezo mazuri kuhusu *Lip Sticks* lakini ninavyoelewa mimi wanawake hawatumii *Lip Sticks* peke yake wanatumia na wanja ambao unapendezesha macho yao. Je, wanja ambao unauzwa Tanzania umepitia *TBS? (Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri! Aah, ngoja kidogo, nadhani swali hili linahusu Wizara ya Afya, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA (k.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA):** Mheshimiwa Spika, sheria iliyoanzisha Mamlaka ya Chakula na Dawa imetoa uwezo kwa mamlaka hiyo kuchunguza na kujiridhisha na usalama wa vyakula, dawa na vipodozi vyote vinavyoingia ndani ya nchi hii. Kwa maana hiyo basi, nataka nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba mamlaka hiyo imekuwa inafanya kazi zake za kuhakikisha kwamba vyakula, dawa na vipodozi vyote vinachunguzwa na kuhakikisha usalama wake kabla ya kuruhusiwa ndani ya nchi. Kwa hiyo, naomba niwatoe wasiwasi wananchi wote kwamba vipodozi vyote ikiwemo wanja huchunguzwa kabla ya kupewa kibali cha kuuzwa nchini.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali unakaribiakwisha na maswali yamekwisha. Kabla hatujaendelea kuna matangazo mawili ya vikao vya Kamati. Tangazo la kwanza, Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mgana Msindai, anawaomba wajumbe wawe na kikao chao leo tarehe 13 Aprili, 2004 mara baada ya kikao cha briefing na kikao kitafanyika ukumbi Na.133, ghorofa ya kwanza. Kamati ya pili ni Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Sophia Simba anaomba wajumbe wakutane kuanzia saa kumi jioni chumba Na. 227, ghorofa ya pili. Hivyo ndio vikao vya Kamati vya leo.Sasa kama nilivyoeleza mwanzoni, baada ya kumaliza kipindi hiki cha maswali tunaingia kwenye ule mkutano wa Wabunge wote wa *briefing* ili tupate maelezo mbalimbali na

kubadilishana mawazo. Lakini nafikiri ili tuanze vizuri pengine tungetoa nafasi kwa chai kwanza halafu *briefing* ianze saa tano kamili. *(Makofi)*

Sasa baada ya hapo la mwisho, kwa niaba yenu Waheshimiwa Wabunge niwatambue Wabunge wenzetu wawili ambao wamekuwa Marais wa vyombo vya Kimataifa ambao wametokea miongoni mwetu. Rais wa kwanza tunayemtambua na kumpongeza ni Mheshimiwa Getrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Bunge la Afrika *(Pan African Parliament)*. Mheshimiwa Mbunge wa Pili ambaye naye amekuwa Rais ni Mheshimiwa Mbunge wa Muhambwe, Mheshimiwa Arcado Ntagazwa. Yeye amekuwa Rais wa Baraza Kuu la *United Nations Environmental Programme,* tunampongeza sana. *(Makofi)*

Baada ya kuwapongeza Marais hao wawili, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

*(Saa 04.29 Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Ajira na Mahusiano katika Kazi wa Mwaka 2003 *(The Employment and Labour Relations Bill, 2003)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Ajira na Mahusiano katika Kazi wa Mwaka 2003 *(The Employment and Labour Relation Bill, 2003)* na kwa mujibu wa mabadiliko yaliyoambatanishwa, sasa usomwe mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, kama mtakavyokumbuka, nchi yetu kama zilivyo nchi zingine ulimwenguni kote, imo katika mageuzi ya kiuchumi, kisiasa na kijamii, mabadiliko ambayo yanagusa misingi ya uwajibikaji wetu katika utendaji wa kazi zetu, utamaduni wa kukosoana, ambao unajenga ustawi wa jamii yetu na maendeleo ya Taifa letu kwa ujumla. Mageuzi haya ya kiuchumi yamefungua milango kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, nchi yetu kuwekeza hapa nchini. Kwa kutambua kwamba Tanzania haiishi kama kisiwa, hali hii imeleta msukumo wa kuweka mazingira ndani ya nchi yenye kuvutia na pia kuhimili ushindani. Pia kuna suala zima la utandawazi ambalo nalo limeikumba nchi yetu kwani hili nalo linawafanya waajiri wote wa umma na wa binafsi kujipanga upya. Mabadiliko ya teknolojia nayo yameathiri sana mipango na taratibu za kazi katika sehemu nyingi za kazi. Teknolojia imesababisha watu kuachishwa kazi, kuajiriwa au kujiajiri upya na pia kuwa na taratibu tofauti kabisa za

utendaji kazi. Kwa hiyo basi, pamoja na mazingira mazuri ya utulivu na amani ambayo nchi yetu imekuwa nayo kwa muda mrefu, sheria zetu za kazi zimekuwa ni kikwazo katika kufanikisha kuvutia wawekezaji wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi kirefu kumekuwepo na malalamiko ya waajiri, wawekezaji, wafanyakazi, Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla, kuhusu sheria za kazi kwamba zimepitwa na wakati. Sheria hizi zilitungwa kati ya mwaka 1949 na 1967. Katika kipindi chote hicho yamekuwepo mabadiliko makubwa katika nyanja ya kiuchumi, kisiasa na kijamii, mabadiliko ambayo yameendelea kutokea nchini na ulimwenguni yanayogusa nyanja ya kazi na ajira. Mabadiliko haya yamesababisha sheria za kazi zilizopo kutokukidhi mahitaji ya sasa kwa ufanisi. Mabadiliko hayo ni pamoja na nafasi ya Serikali kujiengua kuwa mwajiri mkuu na badala yake sekta binafsi kuchukua nafasi hiyo, matakwa ya mikataba mbalimbali ya Shirika la Kazi Duniani *(ILO),* ambayo nchi yetu imeridhia na nchi nyingi za *SADC* na zile za Afrika Mashariki, kuangalia upya sheria zao za kazi ili kujenga upya soko la ajiri kwa nchi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuwepo uhuru wa Vyama vya Wafanyakazi, kuundwa vyama vyao bila kuingiliwa na Serikali au kuwa jumuiya za chama cha siasa kama ilivyokuwa huko nyuma. Ukomeshaji wa ubaguzi katika ajira na malipo, ukomeshaji wa ajira na ajira mbaya ya watoto, kulindwa kwa haki za msingi za wafanyakazi na utatanishi wa nafasi ya vyama sehemu za kazi katika kipindi cha vyama vingi na kadhalika, yaani vyama vingi vya wafanyakazi siyo vyama vingi vya siasa. Mabadiliko haya yalilazimu Serikali kufanya mabadiliko ya sera za sheria katika nyanja za kazi na ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi za mwanzo zilifanyika mnamo Mei, 1986 wakati Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, ilipoielekeza Tume ya Kurekebisha Sheria kufanya utafiti na kupendekeza mfumo muafaka. Tume hiyo iliwasilisha mapendekezo yake Juni, 2001 na suala moja ambalo lilionekana waziwazi ni kwamba, sheria zenyewe zilikuwa zimesambaa katika majarida mbalimbali na ilikuwa ni kazi ngumu wakati wa kuzitumia. Sheria zingine zilikuwa hata zikipingana na wajibu wa Tanzania katika kutekeleza majukumu yake ya Kimataifa. Pamoja na kazi hii nzuri ya Tume kukamilika, mabadiliko ya kasi yaliyotokea baada ya utafiti huo yaliilazimu Serikali kuunda upya Kamati Maalum ya Utatu ili iweze kutoa mapendekezo maalum. Shughuli hii ilifanyika kwa kushirikiana na taasisi zifuatazo: Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Rais, Menejimenti na Utumishi wa Umma, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi ya Waziri Mkuu, Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi, Muungano wa Vyama vya Waajiri, Viongozi wa Vikundi vya Wafanyabiashara, wasomi na watu binafsi wenye uzoefu wa masuala ya kazi. *(Makofi)*

Kamati Maalum hii ilipewa hadidu za rejea zifuatazo: Kuangalia upya sera za soko la ajira, kuangalia upya sheria za kazi na kuangalia sheria za taasisi zinazosimamia masuala ya kazi. Kamati Maalum ilipoanza kazi ilikubaliana kuwa pamoja na kwamba kuna haja ya kuangalia upya mambo yaliyotajwa hapo juu pamoja na kwamba kila mtu

anatoka katika sehemu tofauti ya uwakilishi lakini waliamua waongozwe na kile ambacho wataona kuwa ni chenye maslahi ya nchi na ndiyo wakabuni kauli mbiu ya Nchi kabla ya Jimbo *(Country Before Constituency)* na pia waliamua kuziandika upya kabisa sheria za kazi badala ya kuziba viraka.

Kamati iliamua kuwa katika kupima sera na sheria za sasa za kazi, watumie vigezo vya jinsi vinavyokidhi matarajio kama ifuatavyo: Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Katiba ya Umoja wa Taifa *(The African Charter),* mapendekezo mbalimbali toka Mahakama ya Rufaa na Mahakama ya Kazi, Mikataba ya Shirika la Kazi ya Duniani *(ILO)* iliyoridhiwa na Bunge na inayokusudiwa kuridhiwa na mwelekeo wa uainishaji wa sheria za kazi katika nchi za *SADC* na Afrika Mashariki. Kamati ilifanya kazi kwa kuwaomba watalaam waandike makala za mada zenye kulenga maeneo waliyokusudia ambapo makala hizi ndiyo zilikuwa msingi wa uundaji upya wa sera na sheria za kazi.

Hatua ya pili ya utendaji kazi ya Kamati hii ilikuwa ni ya majadiliano. Majadiliano haya yalifanywa katika ngazi tofauti. Ngazi ya kwanza ilikuwa ngazi ya Kamati yenyewe kwa kushirikisha wadau wenyewe wote muhimu hasa Vyama vya Wafanyakazi na Vyama vya Waajiri. Ngazi ya pili ilikuwa ni majadiliano ya bayana *(Public Hearing)* katika sehemu mbalimbali za nchi zikiwemo Dar es Salaam, Arusha, Tanga, Mwanza, Mbeya na Dodoma. Hatua ya tatu ni kwamba, Taasisi zisizo za Serikali ziliandikiwa barua maalum na kuombwa zitoe mawazo yao, baadhi yake zilitoa na Vyuo Vikuu vyote nchini viliandikiwa vikaombwa kutoa mawazo yao navyo vikatoa. Hatua ya nne ni kuwa baada ya majadiliano haya, Kamati iliunda Kamati Ndogo ya Watalaam ili kuandaa mapendekezo, mapendekezo haya yalijadiliwa tena na Kamati Maalum na kuzaa Muswada uliolenga kusomwa mara ya kwanza Novemba, 2003 hapa Bungeni.

Baada ya kusomwa kwa Muswada kwa mara ya kwanza, baadhi ya wadau walihitaji kuweka msisitizo maalum katika maeneo fulani fulani na kwa hiyo, Serikali ikaitisha semina maalum Mjini Morogoro iliyoshirikisha vyama vyote vya wafanyakazi, vyama vyote vya waajiri, Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii ya Bunge, Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Katiba na Sheria ya Bunge na wananchi binafsi. Maoni mbalimbali yalitolewa na baadhi ya haya yamezingatiwa katika kuboresha Muswada huu zaidi. Baadaye Muswada huu pamoja na yale yaliyozingatiwa kutoka semina ya Morogoro baada ya kuidhinishwa na Serikali, ulipelekwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, ambayo nayo iliita tena wadau wote wakuu na kuwashirikisha tena kwa maboresho zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusisitiza hapa ni kwamba, Muswada huu umejadiliwa sana na wadau wote wanaohusika katika sekta hii ya sheria za kazi. Madhumni makubwa ya Muswada huu ni kuweka sheria, kanuni, miundo na mifumo ya shughuli za kazi ambazo zinatokana na sera inayolenga mambo yafuatayo: Kwanza kabisa, kulinda haki, maslahi na wajibu kwa waajiri na wafanyakazi. Pili, kuwa na mfumo wenye urahisi wa kubadilika kwa namna ambayo inaleta uwiano kati ya lengo la kukuza uchumi na kulinda haki za wafanyakazi. Tatu, kuwa na sheria nyepesi zenye

kueleweka na kutekelezeka kwa watumiaji na nne, kukuza nafasi za ajira na ujasiliamali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu ambayo ni kuhakikisha haki za msingi *(Core Rights)* kama vile kuondoa ubaguzi katika ajira na mishahara, kukomesha ajira mbaya sana ya mtoto na kadhalika zinatekelezwa. Aidha, Muswada umeyazingatia makundi maalum *(Valuable Groups)* kuwa yanalindwa katika mfumo wa kazi, sheria na kanuni za utumishi wa umma zinatambulika ilimradi tu hazipingani na matakwa ya sheria hii mpya. Kuwezesha kukidhi mahitaji ya mifumo mipya ya ajira.

Sheria pia inaruhusu utaratibu laini wa mipango ya kazi na wastani wa saa za kazi *(flexibility of working arrangement and averaging of working hours)* kwa makubaliano ikizingatiwa pia kulinda afya na usalama wa wafanyakazi, familia zao na maslahi ya Taifa. Muswada pia umezingatia kulinda viwango vya kazi kama vile mishahara, likizo na kadhalika. Pia sheria inaweka bayana uhuru wa vyama vya wafanyakazi, wajibu wa vyama sehemu za kazi na mahusiano sehemu za kazi zenye vyama vingi, yaani vyama vingi vya wafanyakazi. Isitoshe kupunguza migogoro ya kikazi kwa kuimarisha kaguzi za kazi na uchukuaji wa hatua pale panapotokea ukiukwaji wa sheria.

Sheria vile vile imeweka mifumo inayowezesha majadiliano, mashauriano na ushirikishwaji wa sehemu ya kazi, mfano mzuri ni mashauriano wakati wa upunguzwaji wa wafanyakazi. Vile vile haki ya kugoma kwa wafanyakazi imewekwa bayana pia uhuru wa waajiri kuwafungia nje wafanyakazi kama silaha ya majadiliano ili kupata suluhu kwenye migogoro ya kikazi imetambulika. Utaratibu wa kuwa na kima cha chini cha mishahara na vima vya chini vya mishahara kisekta umetambulika. Sheria mpya inayomlinda mfanyakazi asiachishwe kazi bila uhalali na imebainisha mazingira na taratibu za kuvunja mikataba ya ajira. Pia haitaruhusiwa mfanyakazi kufukuzwa kazi kwa msingi wa uonevu au ubaguzi. Mwisho, migogoro ya kikazi, madai ya stahili na masuala ya nidhamu yasiyotatulika kwa njia ya mazungumzo, vitawasilishwa katika kamisheni ya usuluhishi na maamuzi *(Conciliation and Arbitration Commission)* badala ya kupitia kwenye Mabaraza ya Usuluhishi ambayo sasa yamefutwa.

Usuluhishi wa mgogoro unaposhindana, suala hilo litawasilishwa kwenye Mahakama ya Kazi kwa uamuzi wa tuzo pale ambapo mgomo hauruhusiwi. Aidha, yule asiyeridhika na uamuzi wa Kamisheni kuhusu *style* hii au nidhamu, atakata rufaa Mahakama ya Kazi badala ya vifaa kwenda kwa Waziri. Rufaa ikitoka hapo itapelekwa Mahakama ya Rufaa. Ili kurahisisha matumizi ya sheria mpya, mapendekezo yametolewa kuwa sheria mpya zisomeke pamoja na *course of good practice, guidelines and models.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu una sehemu kuu tisa. Sehemu ya kwanza inahusu kifungu cha kwanza hadi cha nne na hii inahusu masuala ya utangulizi yanayohusiana na jina la Muswada, kuanza kutumika kwa sheria, mipaka ya sheria na ufafanuzi wa maneno na misemo yenye maana maalum katika sheria inayopendekezwa. Sehemu ya pili, ni kifungu cha 5 hadi 11, inahusu haki na kinga za msingi kwa jamii kwa mfano ajira kwa watoto na ajira za kulazimishwa na ubaguzi katika ajira, misingi

mbalimbali inakatazwa, aidha uhuru wa kuunda vyama vya wafanyakazi na waajiri umetolewa katika sehemu hii. Sehemu ya tatu, inahusu kifungu cha 12 hadi 44, inahusu viwango vya ajira *(Employment Standards),* ambapo masuala ya saa za kufanya kazi, ujira unaostahili na ukame wa ajira, yamezungumziwa.

Sehemu ya nne, inahusu kifungu cha 45 hadi 58, hii inahusu vyama vya wafanyakazi, vyama vya waajiri na mashirikisho ya vyama vyao. Masharti ya msajili kwa vyama hivyo, majukumu yao pia yameelezwa, mambo yanayohusu muungano wa vyama vilivyosajiliwa, kufutwa kwa usajili nayo imeshughulikiwa katika sehemu hii. Sehemu ya tano, ni kifungu 59 mpaka 74, inahusu haki za vyama vilivyoungana, sehemu ya sita inahusu ubishani, mashauriano ya pamoja baina ya vyama vya wafanyakazi na waajiri.

Sehemu ya saba, kifungu cha 75 hadi 85, inaweka masharti kuhusiana na haki na mipaka ya migomo na kufungia nje wafanyakazi *(Strikes and Lockouts).* Sehemu hii pia ina inazungumzia utaratibu wa kujiunga na migomo halali au ufungiaji nje wafanyakazi kihalali. Sehemu ya nane kifungu 86 hadi 95, inaweka masharti yanayohusu usuluhishi migogoro ya kikazi ambapo mambo yanayohusu migogoro yenyewe utaratibu na namna ya migogoro hiyo itakavyoshughulikiwa na uamuzi katika usuluhishi inavyoweza kutolewa yameelezwa.

Sehemu ya tisa kifungu 96 hadi kifungu 103, inahusu masharti ya ujumla ambapo waajiri na wafanyakazi wanapaswa kutunza kumbukumbu zao. Katika sehemu hii pia adhabu kwa makosa mbalimbali chini ya sheria hii yamependekezwa. Waziri pia amepewa mamlaka ya kutunga kanuni za kusaidia katika utekelezaji wa sheria hii. Aidha, katika sehemu hii pia imependekezwa kufuta baadhi ya sheria zilizomo katika jedweli na kurekebishwa zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inaamini Muswada huu ukipita tutaweza kuzipata sheria ambazo kwa kiasi kikubwa zinakidhi matarajio ya waajiri na wawekezaji na wakati huo huo kulinda haki na maslahi ya wafanyakazi. Sheria hizi pia zitawasaidia wafanyakazi kujipanga upya katika mazingira mapya ya ajira kwa kutambua kuwa haki bila kuzingatia wajibu utaliangamizi Taifa. Changamoto kubwa tuliyonayo hapa nchini kama Taifa kwa hivi sasa ni ukosefu wa ajira kwa vijana wetu. Sheria hizi zikipita zitaweka mazingira yatakayoruhusu kukua na kuongezeka kwa ajira ndani ya nchi yetu. Kuandaa mazingira ya aina hii ni wajibu wa Serikali na vyama vya wafanyakazi vinavyojua wajibu wake kwa Taifa lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kumaliza kutoa hoja yangu, naomba nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Sofia Simba, Makamu Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, pamoja na Wajumbe wa Kamati hii, kwa michango iliyoweza kuboresha Muswada huu mpaka ukafikia katika hatua hii. Aidha, shukrani za pekee ziende kwa wadau wa UTATU, wafanyabiashara, watu binafsi waliotoa mawazo yao ya namna ya kuboresha Muswada huu. Ninawashukuru pia Watalaam mbalimbali wa Sheria, Kamishna wa Kazi na Watalaam wake, kwa kazi kubwa ya kuchambua Muswada, masuala mbalimbali ya kazi mpaka kufikia hatua hii.

Ninawashukuru kwa nafasi ya pekee Naibu Waziri, Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir na Katibu Mkuu, Bwana Abubakar Rajab na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, kwa kunipa ushirikiano wa hali ya juu ili kufanikisha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naliomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada huu na kuupitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, orodha ya wachangiaji bado iko wazi kwa yeyote ambaye angependa kuchangia, lakini tulikubaliana kimsingi kwamba, leo Mheshimiwa Waziri awasilishe tu hoja yake na kesho baada ya maswali, Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia Muswada huu ataleta maoni ya Kamati na kuendelea na utaratibu kama ilivyo kawaida.

Sasa baada ya kufika hapo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 11.16 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano*
*Tarehe 14 Aprili, 2004 Saa Tatu Asubuhi)*